

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

04

SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Muda Saa 1:30

Mwaka: 2022

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **matano (5)**
2. Jibu maswali yote katika kila sehemu.

SEHEMU A (Alama 30)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Jibu vipengele (i) na (v) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuiandika kwenye kisanduku ulichopewa.
 - i) Ni kifaa gani hutumika kuhifadhia vyakula kuepuka visiharibike?
A. Kabati B. Jokofu C. Chupa D. Hotipoti []
 - ii) Seti ipi **haiwakilishi** aina ya majiko?
A. Jiko la mkaa, jiko la umeme na jiko la mafuta ya taa
B. Jiko la umeme, jiko la mafuta ya taa na jiko la gesi
C. Jiko la mkaa, jiko la umeme na jiko la gesi
D. Jiko la umeme, mkaa na moto []
 - iii) Ni kifaa kipi hutumika kupima uzito sahihi wa sukari?
A. Kikombe B. Sahani C. Mzani D. Silinda kipimo []
 - iv) Ni sifa ipi ya viumbe hai hutofautisha mimea na wanyama?
A. Kutoa uchafu B. kufa C. Kujongea D. Kukua []
 - v) Nini kazi ya mashine?
A. Kurahisisha kazi C. Kuzalishia bidhaa
B. Kufanyia mawasiliano D. Kunyanyua mizigo []
2. Jibu vipengele (i) hadi (v) kwa kuoanisha maelezo kuhusu dhana mbalimbali za nishati ya joto katika **Orodha A** na dhana husika katika **Orodha B**.

Orodha A	Majibu	Orodha B
i) Namna joto linavyosafiri katika chuma		A. Yabisi
ii) Kusambaa kwa joto katika maji		B. Jua
iii) Namna joto la jua linavyofika duniani		C. Moto
iv) Maada inavyosafirisha joto kwa haraka		D. Mnururisho
v) Chanzo cha asili cha joto		E. Mpitisho F. Msafara G. Vimimika

3. Jibu vipengele (i) hadi (v) kwa kuchagua jibu sahihi kutoka katika kisanduku na kuliandika katika nafasi uliyopewa.

Oksijeni, Chakula, Maji, Hewa, Ardhi, Kabonidayoksaidi, Mimea

- i) Ni gesi ipi hutumiwa na mimea kama malighafi? _____
- ii) Kipi ni matokeo ya muunganiko wa gesi mbalimbali? _____
- iii) Nini chanzo cha chakula kwa viumbe hai? _____
- iv) Ni aina ipi ya gesi inahitajiwa moja kwa moja na viumbe hai? _____
- v) Nini chanzo cha virutubisho kwa ajili ya kazi mbalimbali za mwili?

SEHEMU A (Alama 20)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

4. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu vipengele (i) hadi (v) kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi uliyopewa.

Tunaweza kuyaona maji tunayotumia ni salama kwa macho, lakini yasiwe salama kwa afya zetu. Hii ni kwa sababu maji yanapotiririka ardhini huchukua udongo na wakati mwingine huchukua vijidudu vya magonjwa. Kwa hiyo, tunashauriwa kuchemsha maji ili kuu vimelea vya magonjwa. Baada ya kuchemsha, inatupasa kuyachuja kwa kutumia kitambaa safi ili kuondoa uchafu. Aidha, maji yaliyochemshwa na kuchujwa huhifadhiwa katika chombo safi na chenye mfuniko ili yasichafuke. Haya sasa ni maji safi na salama.

Maswali:

- i) Kwanini ni muhimu kuchemsha maji?
- ii) Ni kwa namna gani maji hupata vijidudu?
- iii) Nini kifanyike ili kufanya maji yawe safi na salama?
- iv) Kifaa gani hutumika kuchuja maji?
- v) Ni kwanini maji huhifadhiwa katika chombo chenye mfuniko?

5. Chunguza picha zifuatazo kisha jibu vipengele (a) and (b)



- a) Nini majina ya vifaa vinavyoonekana katika picha?
i) _____
ii) _____
- b) Ni ugonjwa gani huambukizwa kwa sababu ya kushirikiana katika kutumia vifaa hivyo?
- c) Ni njia gani hutumika kumbaini mtu aliyeathirika na ugonjwa wa ulioutaja katika kipengele (b)?
- d) Ni njia ipi nyingine maambukizi ya ugonjwa ulioutaja katika kipengele (b) hutokea?
- e) Kwanini inashauriwa tusimtenge mtu anayeugua ugonjwa ulioutaja katika kipengele (b)?